**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OWM-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**

**SHULE YA SEKONDARI ZIMBWINI**

**MKUU WA SHULE: +255685613634**

**MAKAMU: +255683620073/0766774667**

**S.L.P 45**

**KIBITI-PWANI**

taalumazimbwini@gmail.com TANZANIA

**Mzazi/mlezi wa mwanafunzi………………………………………**

**S.L.P………………………..**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ZIMBWINI HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI MKOA WA PWANI.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka …... na atasoma tahasusi ya PCB

   Shule ya sekondari Zimbwini ipo mkoa Pwani,wilaya ya kibiti umbali wa kilometa 136 kutoka jiji la Dar es Salaam.Kwa wanafunzi wanaotoka mikoani wafike stendi ya mabasi Mbagala Rangi tatu jijini DSM ndipo watapata Usafiri wa basi kutoka jijini DSM hadi kibiti stendi kwa nauli ya 9000/= na wanafunzi wanaotoka mikoa ya Lindi na Mtwara washukie kibiti stendi.Ukifika stendi ya kibiti utaletwa hadi shuleni kwa usafiri wa pikipiki kwa nauli ya shillingi 1500/=.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe ……….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……….. Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo A-F

A. Maelekezo maalumu ya kujiunga na shule
B. Michango mbalimbali ya shule
C. Sheria ,kanuni na taratibu za shule
D. Fomu ya afya (mwanafunzi apimwe na ijazwe na daktari aliyemhudumia)
E. Ahadi/kiapo cha mwanafunzi
F. Vitabu

## A. MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE: -

### 1. SARE

**SARE YA SHULE**

i. Sare ya shule hii kwa wasichana ni sketi mbili DRAFT, mshono wa ‘’V’’ yenye urefu hadi chini iguse viatu.
ii. Mashati rangi nyeupe mawili ya mikono mirefu au nusu kanzu mbili kitambaa cha harua kwa wanaovaa hijab.
iii. Rangi ya hijab (kijuba) ni rangi nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv. Sare ya michezo ni trucksuits moja rangi ya blue kwa wasichana na raba rangi nyeupe.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga Kamba vyenye visigino vifupi.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe.
vii. Sweta moja rangi ya bluu.
viii. Nguo za kushindia (shamba dress) sketi rangi nyeusi mshono wa ‘’V’’ na juba rangi nyeupe au pink kwa wanaovaa hijab.
ix. T-shirt rangi Blue yenye kola Nyeupe yenye nembo ya shule moja au zaidi kwa ajili ya kuvaa darasani kwa siku maalum na masomo ya jioni (Inapatikana shuleni kwa anayehitaji)
x. Sketi nyeusi moja mshono wa ‘’V’’ yenye urefu hadi chini iguse viatu utaishona nyumbani na utavaa siku ya kuja kuripoti shuleni.

**KITAMBAA CHA SKIRT ZA WANAFUNZI**



**ANGALIZO: Vifaa tajwa hapo juu vinapatikana katika duka la shule kwa atakayehitaji, ili kukurahisishia upatikanaji wa vitambaa vyenye mfanano wa rangi na urefu unaotakiwa ili kuepusha kutofautiana rangi. Ukishona kitambaa kilichotofauti na wenzako utapata hasara ya kushona nyingine.**

2. **MAHITAJI YA BWENI: -**
   - **i.** **G**odoro la futi 2.5 kwa 6.
   - **ii.** Mashuka rangi ya sky bluu jozi 2, foronya ya godoro 1, chandarua rangi nyeupe kimoja.
   - **iii.** Nguo za ndani za kutosha
   - **iv.** Kandambili (bata/bora) kwa ajili ya kuogea na sandal za kimasai zisizo na urembo kwa ajili ya kushindia.
   - **v.** Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko, na kikombe, hotpot moja na chupa ya chai moja).
   - **vi.** Ndoo 2 ndogo (lita kumi) zenye kifuniko.
   - **vii.** Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili (tranker)
   - **viii.** Kwanja 1, jembe 1, mopa 1, mafagio 2 wa ndani na fagio la wima la chelewa la mpini.

3. **MAHITAJI YA TAALUMA**

i. **Ream (A4)** ya karatasi mbili (2) kwa mwaka
ii. **Nakala za cheti c**ha kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa.
iii. Madaftari makubwa 10 (counter book 3 quire)
iv. Scientific calculator (CASIO fx-991) na graph pad moja
v. Kwa wanafunzi wa PCB alete dissection kit kwa ajili ya kujifunzia
vi. Faili mbili kwa ajili ya kuifazia mitihani na kumbukumbu zingine “folder file”
vii. Kwa wanafunzi wa sayansi PCB wanatakiwa kuwa na koti la maabara (lab coat) kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo
viii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha ime ambatanishwa)

**ANGALIZO: mwanafunzi anaweza kununua vitu hivi katika duka la shule ili kukwepa gharama za usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mikoa ya mbali.**
**Kila mwanafunzi anatakiwa kufungua akaunti yake binafsi ya benki CRDB au NMB kwa ajili ya kutunza fedha zake za nauli na mahitaji yake madogo madogo ukija shule utaelekezwa namna ya kufungua, uje na picha za passport size mbili. pia unatakiwa kuwa na Bima ya Afya CHF au NHIF.**

## B. MICHANGO MBALIMBALI

### a) Michango yote ya shule ilipwe Benki

| Na | Aina ya Mchango | kiasi |
|---|---|---|
| **1.** | Mchango wa uendeshanji wa shule | **65,000/=** |
| **2.** | Tahadhari | **5,000/=** |
| **3.** | Nembo | **5,000/=** |
| **4.** | Kitambulisho cha shule | **5,000/=** |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**Michango yote ya shule ilipwe kupitia benki ya NMB akaunti namba 21301100040 Jina la acounti ni ZIMBWINI SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT Jina la mwekaji pesa liwe jina la mwanafunzi na si vinginevyo.**

**Mwanafunzi aje na hati ya malipo ( Bank pay slip) wakati wa kuripoti shuleni.**

## C. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti. Mambo hayo ni pamoja na;

1.1 Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujmla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule na mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule, unatakiwa kuwa na nywele fupi za kuchana na kitana kidogo kwani haturuhusu kusuka nywele;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari wawapo shuleni;
xi. Huruhusiwi kufanya sherehe yoyote ile eneo la shule bila kibali cha Mkuu wa Shule.

**MUHIMU**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anaeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa . Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa ya kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (msiba au ugonjwa)**

### 1.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:

**i.** Wizi
**ii.** Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro
**iii.** Kugoma na kuhamasisha mgomo;
**iv.** Kutoa lugha chafu au maneno ya uchonganishi kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujmla;
**v.** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
**vi.** Kutoroka kwenda nje ya mipaka ya shule, kukaa au kupita maeneo na njia zisizoruhusiwa;
**vii.** Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya;
**viii.** Uvutaji wa sigara;
**ix.** Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa;
**x.** Kupata ujauzito au kutoa mimba au kusababisha mimba;
**xi.** Kukwepa kazi za shule, vipindi vya masomo na kujificha mahali pasipo julikana;
**xii.** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi;
**xiii.** Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
**xiv.** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu au sehemu ya simu ya mkononi kama vile laini, charger, earphone, headphone, memory card, tablet, ipad na smartwatch katika mazingira ya shule.
**xv.** Kuvuruga Amani na usalama wa watu katika mzingira ya shule.
**xvi.** Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa taifa;
**xvii.** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
**xviii.** Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
**xix.** Kufanya mikusanyiko na mikutano shuleni bila kibali cha Mkuu wa Shule au Uongozi wa Shule
**xx.** Kumiliki vifaa vyenye ncha kali bwenini

## D. REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART 'A'**

FROM …………………………………

TO THE MEDICAL OFFICER …………………………….

Mr/miss…………………………………………….. (Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time student. The examination should include the following categories (I-III) each category of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl student ineligible for studies.

I. (a) Eye sight (b) Hearing (c) Speech (d) limbs (e) Venereal Diseases (g) Limbs

II. Neuroses

III. Other serious diseases

Date ……………………………..Signature……………………………….

**PART B.**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government Medical officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physical fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I. (a) Eyesight…………………………………. (b) Venereal Disease……………………….
(c) Hearing …………………………………... (d) Leprosy………………………………..
(e) Speech ……………………………………. (f) Limbs…………………………………...

II. Neuroses……………………………………….

III. Other serious disease…………………………..

IV. Pregnancy ……………………………………..

Date…………………………………………….Signature………………………………….
Station…………………………………………….Designation…………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OR-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI**

**SHULE YA SEKONDARI ZIMBWINI**

**E.** AHADI/KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi …………………………………..ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI ZIMBWINI KIDATO CHA TANO mchepuo wa …………….mwaka 2025 ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na shule ya sekondari ya Bweni Zimbwini.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu,nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania,familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu,familia yangu na kwangu pia.hivyo ninaahidi kuwa,nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo chaguliwa kusoma
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa,nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi /mlezi wangu
…………………………………. (jina la mzazi) kwa ajili ya hatua Zaidi
Saini ya mwanafunzi ……………………..Tarehe……………………..

i. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI
Mimi …………………………………. Ninakubali mtoto wangu …………………..
Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Zimbwini mwaka 2025 .Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.Anuani yangu ya kudumu ni ………………………simu…………………………iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini ya mzazi/mlezi …………………….tarehe……………………..

ii. MWANAFUNZI
Jina la mwanafunzi……………………………..admision Na……………..
Kidato ………………………mchepuo………………mwaka…………….
Tarehe ya kuzaliwa…………………….Mahali ulipozaliwa………………..
Kabila la mwanafunzi…………………..Uraia wa mwanfunzi………………
Tarehe ya kujiunga na shule ya sekondari ya Zimbwini …………shule aliyotoka ya sekondari…………..masomo utakayokuja kusoma……………kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu………………..
Je unarudia kidato……………....kwa nini................................
Dini ya mwanafunzi………………..Dhehebu………………….
Anwani ya kudumu ya mwanafunzi S.L.P……..
Wilaya …………..Mkoa…………….Tarafa……………….kata…………………
Kijiji………………Namba ya nyumba……………………simu nyumbani…………………….simu ya ofisini…………..

iii. BABA
Jina la Baba…………………… je,yu hai?..........
Kabila la baba…………………Anwani yake ya sasa…………kazi yake…………mwajiri wake……………….

Dini ya baba ………………………..dhehebu…………….
Je,baba na mama wanaishi pamoja?............................simu ya baba……………….na ya kazini…………………….

iv. MAMA
Jina la mama ………………………………………
Je,yu hai?......................... kabila la mama……………
Ameajiriwa/amejiajili………………………….
Mwajiri wake………………………….
Anwani yake ya sasa…………………………
Dini ya mama……………….Dhehebu ………………..
Simu ya nyumbani…………………..ya ofisini…………………..

v. MLEZI
Jina la mlezi……………………….kabila la mlezi………………..
Uhusiano na mwanafunzi ukoje………………….....Anwani ya sasa……………….
Kazi yake………………..mwajiri wake………………Dini ya mlezi ……………Dhehebu …………………..
Simu ya nyumbani ………………ya kazini………………….

| PICHA YA BABA | PICHA YA MAMA | PICHA NDUGU WA KARIBU | PICHA NDUGU WA KARIBU |
|---|---|---|---|
| | | | |

Sahihi ya mwanafunzi …………………Tarehe…………………

**F.** VITABU

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na baadhi ya vitabu kutokana na masomo (mchepuo) anayokuja kusoma hapa shuleni.Mwanafunzi atakaguliwa vitabu hivi mara tu atakapofika shuleni

i. COMMUNICATION SKILLS
Kila mwanafunzi lazima aje na kitabu cha somo la communication skills for A-Level.by TIE

ii. BASIC APPLIED MATHEMATICS
Kila mwanafunzi aliechaguliwa kusoma michepuo ya PCB anatakiwa kuja na kitabu cha Basic applied mathematics by TIE

iii. BIOLOGY
Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma biology anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Biology for advanced level secondary school form five by TIE
- Biological science by Robert mudida
- Biological function approach 4$^{th}$ edition
- Understanding Biology for Advanced level By Grenn &Susan Tool

iv. CHEMISTRY
Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma Chemistry anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya.

- Chemistry for advanced level secondary school form five by TIE
- Physical chemistry by CHAND
- Modern chemistry ABC of class XI party I and II by Dr .S.P Jauhar
- Organic chemistry for advanced level secondary school
- In organic chemistry for advanced level secondary school
- General chemistry for advanced level secondary school
- Physical chemistry for advanced level secondary school
- Physical chemistry by Chand

v. PHYSICS

Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma Physics anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya.

- Physics for advanced level secondary school form five by TIE
- Physics for advanced level secondary school form six by TIE
- Modern  ABC of physics part I by Satish Gupta
- Modern  ABC of physics part II by Satish Gupta
- S .Chand’s Principles of physics for class XI by V.K.Mehta & Rohit Mehta
- S .Chand’s Principles of physics for class XII by V.K.Mehta & Rohit Mehta

vi. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO by TIE

2. Viambatanisho na fomu muhimu

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali;


ii. Fomu ya maelezo Binafsi kuhusu Historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

iv. Picha nne za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwnafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

v. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa shule 

Jina la Mkuu wa shule ABDULRAHMANI.S.NDUMBOGANI

Muhuri wa Mkuu wa shule…………………………

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko  mahututi hivyo mzazi atume pesa.**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**:

- Mkuu wa Shule 0685613634
- Makamu Mkuu wa Shule 0683620073 /  0766774667
- Mwandamizi Taaluma 0690061160